



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 24 Mei, 2018.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

243. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamekuwa wakifanya kazi zao vizuri katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwalettea wananchi wetu maendeleo. Hata hivyo, Mawaziri pamoja na Manaibu Waziri makaazi yao yamekuwa Unguja tu wakati kuna huduma nyingi zinahitaji uwepo wao Pemba.

- (a) Je, Serikali ina mpango wa kurejesha ule utamaduni wa zamani wa Manaibu Waziri kuhamia Pemba kuwasadia Mawaziri wao.
- (b) Je, Mawaziri na Manaibu Waziri kubanana hapa Unguja na kuziwacha Wizara kisiwani Pemba na Maafisa Wadhamini peke yao, hatuoni kuwa tunazorotesha baadhi ya mambo yanayohitaji uwepo wa angalau Manaibu Waziri.

- (c) Serikali haioni kuwa kuwahamisha Manaibu Mawaziri Pemba kutasaidia kasi ya utendaji kazi wa Serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

67. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa kuwa SMZ imefanya jambo zuri la kununua meli mpya kwa dola milioni 30 sawa na bilioni 70 au kwa tofauti ndogo lakini meli kama za kampuni ya Azam Sea Ferries kama Sea Link 1 na 2 zimegharimu kama dola milioni 8 sawa na bilioni 16 au na kidogo.

- (a) Je, Serikali haioni hasara iliyopata kwa ununuzi wa meli hii hasa ukizingatia tayari hivi sasa meli inahitaji marekebisho makubwa.
- (b) Je, ni hatua gani SMZ imechukua kwa watendaji kutokana na hasara iliyopatikana juu ya uharibifu huku ikisadikiwa kuwa hata "*log book*" ya safari za meli ilikuwa haiwekwi kama sheria inavyowataka.
- (c) Je, meli ya Mapinduzi II imekatiwa BIMA.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

16. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Mnamo tarehe 8/03/2018 katika maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani vyombo vya habari vimeripoti matukio ya wanawake kudhalilishwa kingono wakiwa makazini, ambao taarifa zimefafanua kuwa wapo baadhi ya wanawake hawapatiwi kazi mpaka watowe rushwa ya ngono.

- (a) Je, Serikali inazo takwimu za matukio mangapi ya udhalilishaji wa kingono kwa wanawake hasa wanaoombwa rushwa za ngono kwenye ajira.

- (b) Hatua gani zinachukuliwa kuwadhibiti waajiri wanaojihusisha na vitendo vya kuwaomba wanawake rushwa ya ngono kwenye ajira.
- (c) Wanawake wanakumbana na kadhia hii wanatakiwa wafanyaje pindi inapotokea wameombwa rushwa ya ngono.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

252. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Katika malengo yake ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018 Wizara ilijipangia kuwaendeleza wavuvi vijana kuvua katika bahari kuu na kufanya utafiti juu ya kutambua maeneo ya uvuvi yenye idadi kubwa ya samaki.

- (a) Je, Wizara yako imefikia wapi.
- (b) Je, ni vijana wangapi waliofaidika na suala hili.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

21. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Wakati kipindi cha mvua za masika kinakaribia kuanza Serikali imetoa tahadhari kwa wananchi ambao wamejenga kwenye maeneo yenye mabonde kuhama ili kuepukana na athari za mvua hizo.

- (a) Je, maeneo yaliyotengwa kwa ujenzi wa makaazi ya watu ni yepi hasa.
- (b) Je, kwanini Serikali inawavunja watu wakati wameshamaliza kujenga badala ya kuchukuwa hatua mapema kabla hawajaanza.
- (c) Serikali inakuwa wapi tokea mwananchi anatafuta kiwanja, anafanya hatua zote za ujenzi mpaka anamaliza hachukuliwi hatua kama anajenga sipo.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2018/2019.

**Zanzibar,
24 Mei, 2018.**

**(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA.**